

iii- الإقلاب Al-Iqlaab - Kugeuza

Maana yake ni kugeuza kitu na kinavyotakiwa kuwa au kupindua kitu. Katika hukmu za Tajwiyd ni kuigeuza nuwn saakinah au tanwiyn kwa kuitamka kama ni م (miym) pamoja na kuleta ghunnah na pia kuleta إِخْفَاءِ الشَّفَوِي (ikhfaa shafawiy). Hukmu hii hutokea pale tanween au nuwn saakinah inapofuatiwa na herufi moja tu nayo ni ya ب (baa).

Iqlaab inaweza kutokea katika neno moja au maneno mawili.

Katika Misahafu aghlabu hukmu hii imebainishwa kwa kuwekwa م (miym) ndogo juu ya nuwn.

Iqlaab katika nuwn saakinah			
Katika maneno mawili		Katika neno moja	
Inavyotamkwa	Mfano	Inavyotamkwa	Mfano
mimm-ba'di	مِنْ بَعْدِ	layumm-badhanna	لَيُنْبَدَنَّ
mamm-bakhila	مَنْ بَحَلَّ	amm-biuwniy	أَنْبِئُونِي
amm-buwrika	أَنْ بُورِكَ	famm-bajasat	فَأَنْبِجَسَتْ
mimm-ba'dhwin	مِنْ بَعْضِ	yumm-bitu	يُنْبِتُ

Iqlaab katika tanwiyn			
Inavyotamkwa	Mfano	Inavyotamkwa	Mfano
Samiy'a mm - Baswiyraa	سَمِيعًا بَصِيرًا	'utulli mm -ba'da	عُتِلَّ بَعْدَ
'Aliyumu mm - bidhaati	عَلِيمٌ بِذَاتِ	aayaati mm - bayyinaatin	ءَايَاتٍ بَيِّنَاتٍ